

# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



## MFUMO WA KUTUNUKU MATOKEO YA UPIMAJI/MITIHANI YA TAIFA KWA KUTUMIA JUMLA YA ALAMA (DIVISHENI)

### 1.0 UTANGULIZI

Baraza la Mitihani la Tanzania limefanya maboresho ya mfumo wa kutunuku matokeo ya Upimaji na mitihani ya taifa katika ngazi ya elimu ya Sekondari. Maboresho hayo yamefanyika kufuatia maoni ya wadau wa elimu kwa Serikali kuhusu haja ya kuwa na viwango bora vya ufaulu na madaraja yaliyo katika mfumo wa jumla ya alama (Divisheni).

### 2.0 UTARATIBU WA KUTUNUKU MATOKEO YA MITIHANI YA TAIFA

Uchakataji wa matokeo ya Upimaji wa Kidato cha Pili na mitihani ya Kidato cha Nne na cha Sita utazingatia viwango vya alama, madaraja ya ufaulu na utaratibu wa matumizi ya alama endelevu (CA) kama ifuatavyo:

#### (a) Viwango vya alama

##### (i) Kidato cha Pili na cha Nne

GREDI	ALAMA	UZITO WA GREDI (POINTI)	MAELEZO
A	75-100	1	Bora sana (Excellent)
B	65-74	2	Vizuri sana (Very Good)
C	45-64	3	Vizuri (Good)
D	30-44	4	Inaridhisha (Satisfactory)
F	0-29	5	Feli (Fail)

##### (ii) Kidato cha Sita

GREDI	ALAMA	UZITO WA GREDI (POINTI)	MAELEZO
A	80-100	1	Excelent
B	70-79	2	Very Good
C	60-69	3	Good
D	50-59	4	Average
E	40-49	5	Satisfactory
S	35-39	6	Subsidiary
F	0-34	7	Fail

#### (b) Madaraja ya Ufaulu

- (i) Madaraja ya Ufaulu yatakuwa katika mfumo wa Jumla ya Alama (Total Point Grading System) au Divisheni. Mtahiniwa aliyefanya masomo yasiyopungua 7 kwa Kidato cha pili na cha Nne na masomo yasiyopungua matatu ya tahasusi (combination) kwa Kidato cha sita atatumikiwa Daraja la I, II, III au IV kwa kufuata wigo wa jumla ya alama (pointi) kama ifuatavyo:

DARAJA	FTNA (K2) NA CSEE (K4)	ACSEE (K6)	MAELEZO
I	7-17	3-9	Bora sana (Excellent)
II	18-21	10-12	Vizuri sana (Very Good)
III	22-25	13-17	Vizuri (Good)
IV	26-33	18-19	Inaridhisha (Satisfactory)
0	34-35	20-21	Feli (Fail)

- (ii) Mtahiniwa aliyefanya idadi ya masomo pungufu ya saba kwa Kidato cha Pili au cha Nne atahesabiwa kuwa amefaulu kwa kiwango cha chini cha ufaulu wa daraja la Nne endapo atafaulu angalau masomo mawili katika Gredii **D** au somo moja katika Gredi **A, B** au **C**. Aidha, mtahiniwa wa Kidato cha sita aliyefanya masomo pungufu ya matatu ya tahasusi atatumikiwa ufaulu wa chini wa daraja la Nne endapo atafaulu angalau masomo mawili katika Gredi **S** au somo moja katika Gredi **A, B, C, D** na **E**.

#### (c) Matumizi ya Alama Endelevu (CA)

Uwiano baina ya alama endelevu (CA) na Alama za mtihani wa mwisho (FE) utakuwa ni **30:70**. Mchanganuo wa mchango wa alama **30** za CA kwa Kidato cha Nne na cha Sita utakuwa kama ifuatavyo:

CSEE (K4)	
Aina ya Upimaji	Alama
Upimaji Kidato cha Pili	10
Upimaji Kidato cha Tatu (Muhula I, II na Project)	10
Mtihani wa Mock Kidato cha Nne	10
<b>JUMLA</b>	<b>30</b>

ACSEE (K6)	
Aina ya Upimaji	Alama
Upimaji Kidato V (Muhula I, II na Project)	15
Mtihani wa Mock Kidato cha Sita	15
<b>JUMLA</b>	<b>30</b>

### 3.0 HITIMISHO

Utaratibu wa kutunuku matokeo kwa muundo wa madaraja wa jumla ya alama (Divisheni) ulitumiwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kuanzia mwaka 1976 hadi 2013. Hivyo, ni matumaini ya Baraza kuwa mfumo huu utakuwa na tija kwa kuwa unaeleweka vema kwa wadau wa elimu walio wengi.